



Pata Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi kila miaka 5






Pata Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi kila miaka mitano.



Ikiwa una umri wa miaka 25-74, na umewahi kujamiana, unahitaji kupata Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi.



Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi kinaangalia afya ya mlango wako wa uzazi. Mlango wa uzazi UFO ndani uke wako. Ni mlango wa uzazi wako.




Unahitaji kwenda kumwona daktari au muuguzi kupata Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi.



Unaweza kuchagua kwenda na mtu wa kukusaidia.



Unahitaji kukaa katika chumba cha kungoja mpaka daktari yupo tayari.



Daktari ataongea nawe kuhusu Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi.



Unaweza kuhisi wasiwasi au aibu kidogo.



Mtu msaidizi wako anaweza kukaa nawe ukipendelea. Unahitaji kulala kitandani bila kuvaa chupi. Utapewa shuka kukufunika mwili wako wa chini.




Daktari wako atahitaji kuangalia ndani mwili wako kwa kutumia kifaa kinachoitwa speculum. Daktari anaweza kutumia gel kurahisisha kuingiza.



Ni muhimu kujaribu kuhema kwenda ndani na nje, na kupumzisha misuli yenye eneo la siri. Unaweza kuacha kipimo wakati wowote ukiacha kufikia nyumbani.

12




Daktari atatumia speculum kufungua ukeni polepole. Picha hii inaonyesha nini inatokea. Daktari wako atatumia brushhi ndogo kuondoa baadhi ya seli kutoka mlango wako wa uzazi.

13



Seli hizi zinawekwa katika chombo kidogo cha majimaji na zinapelekwa pengine kupimwa.

14



Mwili wetu unajengwa na seli. Virusi vya HPV vinaweza kusa-babisha seli zenye afya za mlango wako wa uzazi kubadilika na kuwa bila afya. Vipimo vya kila mara vya Uchunguzi wa mlango wa uzazi vinaangalia virusi vya HPV na vinaweza kuhakikisha seli za mlango wako wa uzazi zinaendelea kuwa zenye afya.

15




Unaweza kuhitaji mtafsiri kukusaidia na lugha ya Kiswahili, au mafanyikazi au jamaa kukusaidia. Daktari wako atakuambia matokeo ya kipimo chako, au unaweza kumwuliza unapomwona tena.

16



Ikiwa kipimo kinaonyesha kuwa una virusi vya HPV, na/au seli za mlango wako wa uzazi zinakosa afya, daktari wako atakuambia unachohitaji kufanya.

17



Vizuri sana!
Umejitunza afya yako yenyewe.

Hakimiliki ya Serikali ya SA

Unaweza kupakua, kuonyesha, kuchapisha na kutoa nakala yakiwemo ya chapisho hili bila kubadilisha kwa sababu ya kufanya kazi, kusoma, au mafunzo kwa hali ya kuweka ndani kitambulisho cha chanzo na kutoa neno la chapisho.

Siyo kwa matumizi ya biashara au kuuza. Kando la matumizi yoyote yanayoruhusiwa chini ya Sheria ya Hakimiliki 1968, haki zote zingine zinalindwa.

Kizuizi:

Chapisho hili ni mwongozo tu na halikusudiwa kuwa ushauri wa rasmi. Wasomaji wanatolewa moyo kutafuta ushauri wa rasmi kabla kutegemea yoyote yakiwemo hili. Wakati uangilifu umechukuliwa kuhakikisha yakiwemo chapisho hilo ni la sasa hivi wakati wa kuchapisha, Mradi wa SA wa Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi, Idara ya SA Afya, hazichukui wajibu kwa ushahihhi au uzima wa yakiwemo ya chapisho na zinakataa kabisa dhima yote kwa upoteaji au uharibu wowote kutoka kutegemea maelezo yoyote ndani lake.

Niende wapi kwa Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi?

- Daktari wako
- Vituo vya Kutunza Afya GP Zaidi
- Zahanati za SHINE SA
- Vituo vya Afya ya Wanawake
- Huduma za Msingi za Kutunza Afya

Habari kuhusu Kinga cha HPV:

www.hpvaccine.org.au/

www.cancerscreening.gov.au/cervical/resources

Rejesta ya Kitaifa ya Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi:

1800 627 701

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Mradi wa SA ya Vipimo vya Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi

SLP 6, Rundle Mall, Adelaide SA 5000

BaruaPepe: healthcervixscreening@sa.gov.au

www.sahealth.sa.gov.au/cervicalscreening

Huduma za Kufasiri na Kutafsiri:

13 14 50



<https://creativecommons.org/licenses>

FIS: 18016.16. (SWAHILI) May 2019